

Tamko na Sala ya kukataa Laana

Naungama dhambi za mababu zangu na za wazazi wangu na zangu mwenyewe za kuwalaani wengine kwa jina la Uislamu.

Nachagua kuwasamehe na kuwaachilia mababu zangu, baba yangu, maimamu, waliowaongoza wao na mimi kuingia katika laana hizi, na wengine wote walionishawishi kutenda dhambi hii, na kwa ajili ya madhara katika maisha yangu.

Nachagua kuwasamehe wote walionilaani mimi au familia yangu.

Nakuomba unisamehe, Bwana, kwa kukubali na kwa kushiriki katika kuwalaani wengine.

Napokea msamaha wako sasa.

Kwa msingi wa msamaha wako, Bwana, Nachagua kujisameme mimi mwenyewe kwa kuwalaani wengine.

Naikataa dhambi ya kulaani, na laana zozote zilizotokana na dhambi hiyo.

Naikataa chuki dhidi ya wengine.

Naikataa mihemko mikubwa ya kushiriki katika kuwalaani wengine.

Nazivunja nguvu hizi kutoka kwenye maisha yangu (na maisha ya vizazi vyangu) kwa njia ya kazi ya ukombozi ya Kristo juu ya msalaba.

Ninakuomba, ee Bwana, uzivunje laana zote nilizoshiriki, na uwabariki wale niliowalaani kwa baraka zote za Ufalme wa Mungu.

Katika jina la Yesu, vilevile ninakataa na kuvunja laana zote zilizoelekezwa dhidi yangu.

Nayakataa na kuyakana mapepo yote ya chuki na kulaani, na nayaamuru yaondoke kwangu sasa, katika jina la Yesu.

Napokea kufunguliwa na Mungu kutoka laana zote dhidi yangu na familia yangu. Napokea amani, upole, na mamlaka ya kuwabariki wengine.

Naiweka wakfu midomo yangu kunena maneno ya sifa na baraka kwa watu wote katika siku zangu.

Katika jina la Yesu, natamka baraka kamili za Ufalme wa Mungu juu yangu na familia yangu, ikiwa ni pamoja na uzima. Afya njema, na furaha.

Naungama na kukataa miunganiko yote isiyo ya kimungu, vifungo vya nafsi, na mashirikiano na maimamu na viongozi wengine wa Kiislamu ambao waliniongoza kuingia katika matambiko ya Kiislamu, ikiwemo kuwalaani wengine.

Nawasamehe viongozi hao kutokana na sehemu yao katika kuanzisha au kudumisha vifungo vyangi vya nafsi visivyo vya kimungu.

Najisamehe mimi mwenyewe kwa ajili ya sehemu yangu katika kudumisha vifungo hivi vya nafsi visivyo vya kimungu na Waislamu wote ambao nimekuwa chini ya uongozi wao.

Ninakuomba ee Bwana, unisamehe kwa kila dhambi iliyohusika katika kuanzisha au kudumisha vifungo hivi vya nafsi, hususan dhambi za kuwalaani wengine na kuwachukia wengine.

Sasa ninavivunja vifungo vya nafsi vyote na washirika wake kwa viongozi wa Kiislamu [mahsusi nikiwataja kwa majina wale ninaowakumbuka] na kujiachilia kutoka kwao [au majina] na wao [au jina] kutoka kwangu.

Bwana, nakusihii safisha akili yangu kutoka kwenye kumbukumbu zote za miunganiko isiyo ya kimungu ili niwe huru kujitoa mwenyewe kwako.

Ninazikataa na kuzifuta kazi zote za mapepo zinazotaribu kudumisha vifungo vyo nafsi visivyo vya kimungu, na kuviamuru viniache sasa, katika jina la Yesu.

Ninajifunga mimi mwenyewe kwa Kristo Yesu na kuchagua kumfuata yeye peke yake.

Amina.